



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.AC/212/233/218/113

Tarehe: 09.09.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WA MIEZI 08 (LINARUDIWA).

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anakaribisha maombi ya kazi ya Ajira ya Mkataba wa muda wa miezi 08 kwa kada ya Tabibu Msaidizi na Muuguzi II hii ni kutokana na program ya COMMUNITY, SOCIAL RESPONSIBILITY (CSR) inayotolewa na Mgodhi wa Uchimbaji Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu kama ifuatavyo:-

1. TABIBU MSAIDIZI (NAFASI 04) – Ngazi ya Mshahara TGHS A.

(a) SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV ambao wamehitimu Mafunzo ya Miaka Miwili (02) ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate).

(a) Kazi na Majukumu:

- i. Kutoa huduma za Kinga na Tiba
- ii. Kutambua na kutibu magonjwa
- iii. Kutoa huduma ya Afya ya msingi (Primary Health Care)
- iv. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

2. MUUGUZI II (NAFASI 04) - Ngazi ya Mshahara TGHS A.

(a) SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Cheti cha Uuguzi cha Miaka miwili (02) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

(b) Kazi na Majukumu:

- I. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za Afya.
- II. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa Afya katika sehemu yake ya kazi
- III. Kukusanya Takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi

- IV. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani
- V. Kutoa ushauri nasaha
- VI. Kutoa huduma za kinga na Uzazi wa mpango
- VII. Kutoa huduma za Uzazi na Afya ya Mtoto
- VIII. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- IX. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- X. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu, Uzoefu na Ujuzi wake.

MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- iii. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni aidha Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Kitambulisho cha Mpiga kura
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. **Testimonials**", "**Provisional Results**", "**Statement of results**", hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- vi. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**
- vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- viii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 23 Septemba, 2022.**
- ix. **Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale S.L.P 352 Nyang'hwale.**

**MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE.**


Majagi Maiga

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita, Barua pepe: ded@nyanghwaledc.go.tz Tovuti: www.nyanghwaledc.go.tz